

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

☎ Simu: Na : 026 -2702647
📠 Nukushi Na : 026 – 2702203
✉ Email:mkurugenzi@iringamc.go.tz
📘 Facebook: Manispaa iringa 1
🌐 Tovuti:www.iringamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa,
S.L.P 162
IRINGA

31/01/2020

TANGAZO (LIMERUDIWA)

**TANGAZO LA ZABUNI YA
KUTAFUTA MWEKEZAJI KATIKA BUSTANI YA MANISPAA YA IRINGA:
ZABUNI NA LGA/025/2019/2020/NC/08**

1. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inamiliki bustani iliyopo mukhabara na Ofisi za makao makuu ya Halmshauri ya Manispaa. Bustani hii iko katikati ya Mji na ni eneo la wazi na mahususi kwa ajili ya mapumziko ya watu wote likiwa na miundo mbinu muhimu ya maji, umeme, jengo la mgahawa, choo na kituo cha kutolea Habari kwa watalii, (Tourist Information Centre). Eneo hili limesheheni Nyasi, Ukoka, Maua na Miti ya aina mbalimbali, Vyote hivi vikifanya mandhari yake kumpendeza hivyo kuwa kivutio kwa watu mbalimbali ndani ya Manispaa na hata wageni kufika kwa ajili ya mapumziko Chakula na vinywaji.
2. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inawatangazia Wananchi, Makampuni, Taasisi malimbali na vikundi vilivyoandikisha kuleta Maombi ya Zabuni kwa ajili ya uwekezaji katika bustani ya Manispaa.
3. Mchakato wa Zabuni utaadeshwa chini ya utaratibu wa Zabuni za ushindani kwa waombaji wenyeji (**Preference to Local Communities**) kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013, Tangazo la Serikali Na 446 na marekebisho yake na Zabuni ziko wazi kwa waombaji wote wenyeji au vinginevyo kama itakavyoelekezwa katika kabrasha la Zabuni sehemu ya vigezo vya maandalizi ya Zabuni.

4. Waombaji wenye nia na sifa wanaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kununua na kusoma nyaraka za Zabuni katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa S.L.P 162 Iringa, kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi 9:30 jioni siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu.
5. Seti nzima ya makabrasha ya Zabuni yakiwa katika lugha ya Kiswahili inaweza kununuliwa na wazabuni wenye nia kwa kuleta Maombi kimaandishi kwa anuani iliyotajwa katika aya ya nne hapo juu kwa malipo ya Tsh 100,000/= ambazo hazitarudishwa hata kama mwombaji atashindwa Zabuni .Malipo yafanyike kwa hundi au kupita bank kwa Mkurugenzi wa Manispaa. Kwa waombaji walioshiriki katika mchakato wa awali hawatahitaji kulipia tena ada ya maombi ya zabuni, bali watalazimika kuchukua nyaraka ya zabuni kwani ina maeneo yenye marekebisho tofauti na ya awali.
6. Zabuni zote ziambate na kiapo cha dhamana ya Zabuni (Tender Securing Declaration) kwa kuzingatia fomati iliyoainishwa katika Kabrasha la Zabuni.
7. Zabuni zote zitumwe katika Nakala moja halisi na Nakala mbili vivuli zikiwa zimefungwa vizuri kwa lakiri kwenye bahasha bila kuwa na alama yoyote inayoashiria zilikutoka na zitumwe kwa:

KATIBU,
BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA MANISPAA,
S.L.P 162,
IRINGA.

Na zimfikie kabla au ifikapo tarehe 14/02/2020 saa nne kamili asubuhi, Zabuni zitafunguliwa mara tu muda huo utakapowadia mbele ya waombaji au wawakilishi wao watakaohiari kuhudhuria zoezi la ufunguzi wa Zabuni.

8. Zabuni zitakazochelewa kupokelewa, Zabuni zitakazoletwa kwa njia ya kielektroniki, Zabuni ambazo hazijapokelewa na Zabuni ambazo hazitafunguliwa hadharani siku ya ufunguzi wa Zabuni hazitofikiriwa na Kamati ya uchambuzi wa Zabuni hata kwa sababu yoyote ile.



HAMID A. NJOVU
MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA IRINGA

